



Wilaya ya 11 (District 11) ya Colorado Springs

Ujumbe wa Jamii kwa Wanafunzi Wahamiaji Wasio kuwa na Vibali Halali

District 11 inatilia maanani utoaji wa elimu bora na ya ki pekee inayotayarisha wanafunzi ili waweze kufaulu leo na siku zijazo. Kwa uhakika, amri ya Rais, “Uimarishaji wa usalama wa umma ndani ya mipaka ya nchi ya marekani” (Enhancing Public Safety in the Interior of the United States) imesababisha mashaka na wasiwasi baina ya wakaazi wetu. Katika District 11, tunataka kuwahakikishia wanafunzi wetu na familia zao kwamba wamekaribishwa katika shule zetu.

District 11 inajitahidi kudumisha mazingira ya elimu na ufanyakazi ulio salama na pia inadhibitisha uimarishaji na mafanikio ya wanafunzi. Kuweza kufanya hivyo, lazima tu wape wanafunzi na familia zao haki wanazostahili. Sera ya District 11 dhidi ya ubaguzi ina piga marufuku ubaguzi wa mtu yeyote kwa msingi wa ulemavu, taifa, imani, rangi, jinsia, mwelekeo wa kijinsia(kama ilivyoelezwa na sheria za jimbo), asili ya kitaifa, dini, ukoo na umri. District 11 inafuatilia sheria zote zinazohusikia.

Sisi kama District 11 tunajitahidi kuwaunga mkono, wafanyakazi wetu na kuwasaidia kujenga uhusiano zaidi baina yao na familia za wanafunzi na pia kuwasaidia wanafunzi kuipa kipaumbele masomo na mafanikio yao. District 11 pamoja na wafanyakazi wetu tuna fursa ya kutumia rasilimali ambazo zinazotusaidia kutoa huduma maalum kwa wanafunzi. Huduma hizo mbali mbali ni pamoja na kutatua wasiwasi wowote uliosababishwa na amri ya Rais ya hivi majuzi. Wasiliana na mwalimu wako, mwalimu mkuu au shule yako kwa ushauri juu ya rasilimali za kijamii.